

Mkate wa Siku

SIKU
31

NENO LA SIKU

Aug. 2022

SIKU 01 - KUTOKA 23:20a (SUV)

“Tazama, mimi namtuma malaika aende mbele yako, ili akulinde njiani...”

SIKU 02 - ZABURI 139:17 (BHN)

“Ee Mungu, mawazo yako ni makuu mno; hayawezi kabisa kuhesabika!”

SIKU 03 - ISAYA 60:1 (NEN)

“Ondoka, angaza, kwa kuwa nuru yako imekuja na utukufu wa Bwana umezuka juu yako.”

SIKU 04 - YAKOBO 4:8a (SRUV)

“Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi.”

SIKU 05 - KUMB. 33:27a (SUV)

“Mungu wa milele ndiye makazi yako, Na mikono ya milele i chini yako...”

SIKU 06 - 1 SAMWELI 14:6b (BHN)

“Huenda Mwenyezi-Mungu akatusaidia, maana Mwenyezi-Mungu haokoi kwa kutegemea wingi au uchache wa watu.”

SIKU 07 - ZABURI 66:5 (SRUV)

“... Hutisha kwa mambo awatendayo wanadamu!”

SIKU 08 - ISAYA 28:29b (NEN)

“... mwenye mashauri ya ajabu, na anayepita wote kwa hekima.”

SIKU 09 - 2 WAKORINTHO 9:8 (SUV)

“Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;”

SIKU 10 - 1 WAKORINTHO 6:20 (SRUV)

“maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.”

SIKU 11 - MWANZO 18:14a (ONEN)

“Je, kuna jambo lolote gumu lisilowezekana kwa Bwana?”

SIKU 12 - ZABURI 119:130 (NEN)

“Kuingia kwa maneno yako kunaleta nuru, kunampa mjinga ufahamu.”

SIKU 13 - ISAYA 54:14a (BHN)

“Utamarika katika uadilifu, utakuwa mbali na dhuluma, nawe hutaogopa kitu;”

SIKU 14 - YOHANA 14:1 (SUV)

“Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi (Yesu).”

SIKU 15 - WAKOLOSAI 1:16a, 17b (BHN)

“Maana kwake vitu vyote viliumbwa.... vyote huendelea kuwako kwa uwezo wake.”

SIKU 16 - MAOMBOLEZO 3:57 (SRUV)

“Ulinikaribia siku ile nilipokulilia; Ukasema, Usiogope.”

SIKU 17 - ZABURI 18:2a (ONEN)

“Bwana ni mwamba wangu, ngome yangu na mwokozi wangu; Mungu wangu ni mwamba, ambaye kwake ninakimbilia.”

SIKU 18 - ISAYA 51:16a (NEN)

“Nimeweka maneno yangu kinywani mwako na kukufunika kwa uvuli wa mkono wangu...”

– ENDELEA UKURASA UNAOFUATA...

SIKU 19 - WAEFESO 2:21 (SUV)

“Katika yeye jengo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana.”

SIKU 20 - YEREMIA 1:8 (SRUV)

“Usiogope kwa sababu ya hao maana mimi nipo pamoja nawe nikuokoe, asema BWANA.”

SIKU 21 - NAHUMU 1:7 (SUV)

“BWANA ni mwema, ni ngome siku ya taabu; naye huwajua hao wamkimbiliao.”

SIKU 22 - 1 PETRO 2:9 (NEN)

“Lakini ninyi ni taifa teule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu walio milki ya Mungu, mlioitwa ili kutangaza sifa zake yeye aliyewaita kutoka gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu.”

SIKU 23 - WARUMI 8:1 (ONEN)

“Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho.”

SIKU 24 - ZABURI 71:19b (BHN)

“Wewe umefanya mambo makuu mno. Ee Mungu, ni nani aliye kama wewe?”

SIKU 25 - ISAYA 42:3 (SRUV)

“Mwanzi uliopondeka hatauvunja, wala utambi utokao moshi hatauzima; atatoa hukumu kwa uaminifu.”

SIKU 26 - LUKA 10:20b (SUV)

“...bali furahini kwa sababu majina yenu yameandikwa mbinguni.”

SIKU 27 - MATAYO 6:8b (BHN)

“Baba yenu anajua mnayoyahitaji hata kabla ya kumwomba!”

SIKU 28 - WAGALATIA 3:13a (SRUV)

“Kristo alitukomboa katika laana ya torati, kwa kuwa alifanywa laana kwa ajili yetu.”

SIKU 29 - ZABURI 3:8 (SUV)

“Wokovu una BWANA; Baraka yako na iwe juu ya watu wako.”

“SIKU 30 - SEFANIA 3:17 (BHN)

“Mwenyezi-Mungu, Mungu wako yu pamoja nawe yeye ni shujaa anayekuletea ushindi. Yeye atakufurahia kwa furaha kuu, kwa upendo wake atakujalia uhai mpya. Atakufurahia kwa wimbo wa sauti kubwa.”

SIKU 31 - UFUNUO 1:8 (RSUV)

“Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, asema Bwana Mungu, aliyeko na aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi.”

**Makala hii imechukuliwa
kutoka
www.biblesociety.ca © Haki
zote zimeifadhiwa.**

*Tunawashukuru sana kwa kuungana
na sisi kueneza Neno la Mungu hapa
Tanzania na duniani kote kwa ujumla.*

Chama cha Biblia cha Tanzania
16 Hatibu / 9 Barabara, Eneo la Madukani,
S.L.P 175, Dodoma - Tanzania



**Canadian
Bible Society**

10 CARNFORTH ROAD, TORONTO, ON M4A 2S4
TOLL FREE: 1.800.465.2425 EMAIL: INFO@BIBLESOCIETY.CA

WWW.BIBLESOCIETY.CA